

Swahili transcript:

Pia wanawake wa kitanzania wanapovaa mavazi haya ya vitenge, huwa pia wananunua na shanga au urembo ambao unafanana na nguo ile ambayo anavaa. Kwa mfano hapa nilipo nimevaa hii, hii ni wazungu wanasema necklace, lakini tunaita mkufu, ni mkufu ambao umetengenezwa na vitu ambavyo ni vya kiutamaduni, pamoja na hapa mkononi, na hii pia ni bangili, ni bangili ambayo imetengenezwa na watanzania, wametumia vitu ambavyo ni vya kiasili katika kutengeneza. Kwa hiyo ni urembo ambao unapendeza, kama ambavyo mnaniona ni urembo ambao unapendeza, na umeendana na rangi za hii nguo ambayo nimevaa. Kwa hiyo ni vitu ambavyo vinapendeza kwa watanzania walio wengi, wanapenda wakivaa nguo, wavae na, mkufu pamoja na ile bangili au hata hereni pia ziweze kufanana na nguo ambayo ameivaa.

English translation:

Tanzanian women prefer to wear *kitenge* clothes that match the bangles, necklaces and other things. For example, here is what white people call a necklace; we Tanzanians call it *mkufu*. It means the same thing, necklace. This necklace has been made from natural materials. On my wrist is a bangle which has also been made by Tanzanians from natural materials. It is a good decoration and matches this *kitenge* dress. Many Tanzanian women prefer to dress this way, where the dress matches the bangles, necklace and even the earrings.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.